OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
SHULE YA SEKONDARI MUHWANA, S. L. P. 2223, IRINGA
SIMU 0652285454/0755204584

KUMB. NA.MHSS/VOL.V/2017/JIF/11
JINA LA MWANAFUNZI .....
.....
S. L. P .....

YAH; MAAGIZO NA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MUHWANA, WILAYA YA IRINGA, MKOA WA IRINGA

1.0 UTANGULIZI

Nafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa/umepata kibali kujiunga na Shule ya Sekondari Muhwana,kidato 1 2021.Hongera sana kwa jitihada,bidii na maarifa kwenye nidhamu na taaluma;natarajia utafanya vema zaidi katika ngazi ya Sekondari kutimiza ndoto zako kimaisha na matarajio ya Umma.Shule ipo umbali wa kilomita 35 kusini mashariki mwa makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Iringa.Usafiri wa Basi la Mwembamba ama Haisi kutoka Iringa hadi Magulilwa unapatikana katika kituo cha mabasi cha Mlandege na Ipogolo/stendi ya Dabaga kati ya saa 4.00 asubuhi na saa 10.00 jioni.

Muhula wa kwanza 2021 utaanza siku ya jumatatu tarehe 11/01/2021 saa 1.00 asubuhi.

Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe hiyo ukiwa na mzazi au mlezi wako kuandikishwa na kuanza masomo ukiwa umekamilisha taarifa zifuatazo kwa kuziwasilisha kwa msajili Shuleni;

i) Fomu ya ahadi ya kuzingatia Sheria za Shule na taarifa binafsi za mwanafunzi (f.1)
ii) Fomu ya kupima afya ya mwanafunzi (f.2)
iii) Nakala ya Cheti cha kuzaliwa mtoto/mwanafunzi kutoka ofisi ya msajili wa vizazi

2.MASOMO YA DARASANI

Darasani utajifunza masomo 9 kwa lugha ya kiingereza,isipokuwa somo moja tu ambalo utatumia lugha ya Kiswahili, unapoanza kidato cha kwanza na kupimwa kupitia mazoezi,majaribio na mitihani; 1) Civics, 2)History,3) English Language,4)Geography,5)Biology,6)Mathematics,7)Chemistry,8)Physics na 9) Kiswahili. Somo la dini kwa mujibu wa dhehebu lako litafundishwa mara moja tu kwa juma muda wa vipindi.Imani inayoathiri ratiba ya shule na ujifunzaji haikubaliki.

3.0 MAMBO MHIMU YA KUZINGATIA

3.1 SARE YA SHULE.

a) Sare ya Shule ni kitambaa cha rangi ya damu ya mzee,suluari 2 kwa wavulana na sketi 2 kwa wasichana.Suluari mshono wa heshima;modo marufuku kabisa na sketi za mshono wa rindaboksi,pana na ndefu`mini-skirts hazitakiwi kabisa. Mashati 2 rangi nyeupe mikono mirefu kwa wavulana na

wasichana,Sweta rangi ya damu ya mzee,yenye mshono wa V-shingoni. Tai 2 rangi ya kitambaa cha sketi au suluari. Sare ya Hijabu kwa waumini wa kiislam sharti ifanane na sare ya Shule

b) Viatu vya ngozi rangi nyeusi vya kufunga na kamba,kisigino kifupi kwa wanafunzi wa jinsia zote

c) Daftari za counterbooks12 ama zaidi, kalamu za wino/peni za kutosha, na mkebe wa Hisabati na ream paper A4 kwa ajili ya mazoezi ya mara kwa mara.

d) Sare ya michezo; tracksuit rangi ya dark blue kwa wanafunzi wa jinsia zote.

e) Kuwa na chakula cha kutosha na chumba/nyumba ya kuishi kwa kuwa shule ni ya kutwa

f) Socks jozi 2 nyeupe kwa wasichana na rangi kijivu,rangi ya udongo, ama nyeusi kwa wavulana

4.0 BAADHI YA MAMBO AMBAYO HAYARUHUSIWI SHULENI

1) Kumiliki ana kukutwa na simu shuleni,inayojumuisha laini,betri ama housing,hata kwenye chumba ulichopanga simu hairuhusiwi.
2) Kuvaa khanga,kitenge,heleni,mikufu,shanga,bangili,kofia ya mzula au kapelo/Cap,kupaka rangi kwenye kucha,wanja,lipstick nk hairuhusiwi.
3) Kuvaa mitindo ya kihuni na kuonyesha mwenendo na tabia isiyofaa mazingira ya shule na nje kwenye jamii

5.0 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i) Wizi
ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii) Kugoma ama kuhamasisha mgomo
iv) Kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi mwenzake,walimu,walezi na jamii kwa ujumla.
v) Kupigana,kumpiga mwalimu ama mtu wingine yeyote
vi) Kusuka nywele,kunyoa nywele katika mtindo wa kihuni, kufuga kucha ama ndevu.
vii) Matumizi ya pombe,biashara ya pombe,uvutaji wa sigara,pamoja na matumizi ama biashara ya madawa ya kulevya
viii) Uasherati,kuolewa ama kuoa na ushoga/usagaji.
ix) Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa,matendo yanayokiuka taratibu,kanuni na sheria za shule ama Sheria za nchi
x) Kumsababishia msichana ama mwanamke yeyote
xi) Kupata ujauzito ama kutoa mimba
xii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiii) Kumiliki,kutumia ama kukutwa na simu ya mkononi katika mazingira ya kujifunzia ya shule
xiv) Kudharau Bendera ya Taifa ama Wimbo wa Taifa na Alama za Utambulisho wa Taifa
xv) Kuharibu mali ya umma kwa makusudi
xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kuua ama kujiua kwa kunywa sumu ama silaha yoyote ya hatari.

6.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE KWA WANAFUNZI WOTE

Binadamu asilani kuishi ana kukaa pamoja si bure,lazima kuwepo malengo.Aidha taasisi kama hii yetu ina malengo,na ili kufanikisha malengo hayo lazima kuwepo na kanuni na taratibu za kufuata,hususani mwanafunzi wa Muhwana Sekondari.Kanuni na taratibu hizo ni;

A.MAHUDHURIO

Kuthamini muda wa kuwepo mahali anapotakiwa kwa mujibu wa ratiba au maelekezo kutoka kwa uongozi wa shule;

a) Kuwahi kufika na kuwepo mstarini kwa muda uliopangwa,ambapo ni saa 1.00 asubuhi
b) Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo,kazi za mikono na ratiba ya michezo
c) Kuhudhuria mikutano,mfano baraza la shule,ukaguzi wa usafi,vikundi mbalimbali vinavyotambulika kisheria; kama vile vilabu vya masomo,dini nk
d) Kuitikia miito ya dharura mara moja

B.HESHIMA

a) Kuwathamini na kuwaheshimu wana jumuiaya wote
b) Kusimama na kumsalimu mwalimu ama mtu mwingine yeyote anayekuzidi umri anapopita au kuingia mahali ulipo.
c) Kutumia lugha nzuri wakati wote
d) Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wengine katika kazi
e) Kuheshimu na kuthamini kazi za aina zote
f) Kuheshimu Bendera ya Taifa,picha za viongozi wa vyama na serikali,nembo ya Taifa,wimbo wa Taifa na fedha za Taifa
g) Kuheshimu taratibu za mikutano,ofisi za shule,mali binafsi na mali ya umma
h) Kukaa kimya darasani na kutoka nje kwa ruhusa ya mwlimu au kiongozi aliyepo darasani
i) Kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma
j) Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo, ndani na nje ya mazingira ya shule

C.WAGONJWA

Wagonjwa wote wawapo shuleni watapata kibali cha kwenda hospitali kupitia kwa mwalimu wa zamu,darasa ama ofisi ya malezi na nidhamu.

D.USAFI

Usafi ni utamaduni ambao ni sehemu ya maisha,na wajibu muhimu kwa kila mwanfunzi kuzingztia kuwa;

1) Usafi binafsi wa mwili, mavazi yote na mazingira ya kuishi
2) Usafi wa maeneo yafuatayo kama utakavyopangiwa;madarasa, maabara,viwanja na barabara,vyoo nk

TANBIHI;Tafadhali soma kwa makini maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya Mkuu wa Shule……Tarehe……/Mhuri wa Ofisi.

.

IRINGA DISTRICT COUNCIL
MUHWANA SECONDARY SCHOOL, P O. BOX 2223, IRINGA

MEDICAL EXAMINATION FORM- F1

(To filled by a Medical Officer in charge of a Dispensary, Health Centre or Hospital)

Date…….
Full name……Sex; male/female…….
Age……yrs
Blood Count(Red and White)……
Tool examination……
Urine analysis……
Syphilis Test……
Eye Test ……
TB Test……
Ears test……
Chest ……
Spleen……
Abdomen……
ADDITIONAL INFORMATION, eg Physical diagnosis
……
……
……
I certify that the above named person is fit/not fit to pursue her/his studies
Signature……
Designation……
Date……
NOTE;
A parent or pupil's guardian must bring a dully filled form for submission to the school administration as a pre-requisite for admission to school.
No pupil will be enrolled to, without having consulted the medical officer for clinical check up as regards to his or her fitness and, or disabilities.

……
Mwl.Alberto N.Gange
The head o school

SHULE YA SEKONDARI MUHWANA
TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI NA KUKUBALI NAFASI YA MASOMO
F2

A.SEHEMU YA MWANAFUNZI

Majina kamili ya Mwanafunzi……
Tarehe ya kuzaliwa……Mahali……
Uraia…… Umri……Dini……
Anwani ya nymbani……
Kidato anachopokelewa ……Shule atokayo……
Je,wazazi wako wote wapo hai,wanaishi pamoja ama wametengana(Eleza kwa ufupi)
……
……
Saini……Tarehe……
.

B.SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Jina la Mzazi ……Simu Na……
Kazi ya Mzazi ……

C.NDUGU WA KARIBU KWENYE FAMILIA

Jina Kamili	Uhusiano	Simu Na	Mahali anapoishi
1)……	……	……	……
2)……	……	……	……

D.KUKUBALI MASHARTI,KANUNI NA SHERI ZA SHULE

Mimi……wa kidato cha ……ninakubali kujiunga na Shule ya Sekondari ya Muhwana nikiwa mwanafunzi wa kutwa
Nimesoma kwa makini sana masharti,kanuni na taratibu zote, na naahidi kufuata na kuzingatia sheria zote za shule.
Na endapo nitakiuka sheria hizi na maelekezo/maagizo mengine yatakayotolewa,uongozi wa shule uchukue hatua za kinidhamu mara moja dhidi yangu,ikiwa ni pamoja na kurudishwa nyumbani,au kufukuzwa shule

E.USHUHUDA WA MZAZI/MLEZI

Mimi ……nimeshuhudia maelezo na taarifa alizotoa mtoto wangu na kuahidi kuzingatia maadili mema kwa lengo la kutimiza ndoto za kupata elimu bora.Nitamsaidia kwa hali na mali,pamoja na kuwa naye karibu ili kumjengea uwezo.Mtoto anajiunga na shule hii tarehe……

Saini…… Simu Na…… Tarehe……
Cheo……(Mzazi/mlezi)